TANGAZO LA SERIKALI NA. 889 la tarehe 01/11/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1)*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA MSEMBETA YA MWAKA 2024

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa katika Eneo la Msembeta ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali linatangazwa kuwa eneo la upangaji (Mpango wa Urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo la kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Jiji Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

MIPAKA YA ENEO LA UPANGAJI

Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MBT1 yenye majira - nukta 776109.58MS, 9334772.65KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kasikazini -Mashariki katika uelekeo wa KZ89$^{0}$MS kwa umbali wa kilomita 0.642 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MBT2 yenye majira - nukta 776751.88MS, 9334766.25KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa KZ00$^{0}$MS kwa umbali wa kilomita 2.313 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MBT3 yenye majira -

nukta 776761.94MS, 9332453.06KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ58$^0$MG kwa umbali wa kilomita 1.886 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MBT4 yenye majira - nukta 775151MS, 9333433.65KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki katika uelekeo wa KZ35$^0$'MG kwa umbali wa kilomita 1.647 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
28 Oktoba, 2024

DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*